

HUKU NA KULE

1. Peni yangu Andanenga, uwino unapotona
Mantiki huzilenga, na balagha na bayana
Hufaidika malenga, huvurugika akina
Nyege ni kunyegezana, msemu wa Kiswahili.
2. Msemu wa Kiswahili, nyege ni kunyegezana
Maana yaki kamili, "wema ni kutendeanu"
Wasiojua fasili, hunamba nimetukana
Nyege ni kunyegezana, msemu wa Kiswahili.
3. Ni msemu maarufu, ambao shaka hauna
Kwenye kamusi sanifu, funueni mtaona
Niwezeje kukashifu, nami mwana muungwana!
Nyege ni kunyegezana, msemu wa Kiswahili.
4. Ninataja ukurasa, wazi hapa naunena
Soma mbili moja tisa, soma bila ya fitina
Msemu siyo wa sasa, si juzi licha wa jana
Nyege ni kunyegezana, msemu wa Kiswahili.
5. Ushairi kubwa fani, mithili yake haina
Kujua zake bayani, yataka kikubwa kina
Muoneni mwafulani, hata kuku wamguna
Nyege ni kunyegezana, msemu wa Kiswahili.
6. Ulipotamkwa mlo, kaja akitunatuna
Akakabwa koromelo, akabaki kugunaguna
Kabakia lolololo, uzamani umechina
Nyege ni kunyegezana, msemu wa Kiswahili.
7. Alhaji Jitukali, pokea pongezi tena
Kikubwa chako kilili, hapandi yule mtwana
Atuache tule wali, yeye ugali wa dona
Nyege ni kunyegezana, msemu wa Kiswahili.
8. Kaditama wa Busara, na Mbwezi heko kijana
Pongezi ndugu Kagera, Yobu has ante sana
Ndimi Mshairi Bora, kipofu ninaeona
Nyege ni kunyegezana, msemu wa Kiswahili.

(Mshairi Bora)

Amiri A. S. Andanenga (Sauti ya Kiza)

SLP 4775,

Kinondoni Shamba, Dar es Salaam